504

# JARIBIO LA PILI

## DARASA LA NANE - 2020

**Muda: Saa 1 Dakika 40**

# KISWAHILI
## SEHEMU YA KWANZA:
## LUGHA

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA (Soma kwa makini maagizo yafuatayo)**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha chagua jibu lionyeshe katika **KARATASI YA MA JIBU** na wala sio katika kijitabu cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu: -

   **NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye nambari zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **Mfano:**
   **Katika kijitabu cha maswali:**
   **Kutoka swali 16 - 30 chagua jibu sahihi.**

17. Kamilisha methali ifuatayo;
   ***Ukali wa moto ni*** ________
   A. kukuchoma
   B. kuunguza
   C. kuuchochea
   D. kuteketeza

   **Jibu sahihi ni C.**

   **Katika karatasi ya majibu**

   **16.** [A] [B] [C] [D] **17.** [A] [B] [C] [D] **18.** [A] [B] [C] [D] **19.** [A] [B] [C] [D]

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **17**, kisanduku chenye herufi **C** ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

*5042002*

Kijitabu hiki kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.

© compasspress, 2020

FUNGUA KURASA

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 hadi 15. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo kati ya yale uliyopewa.***

_____1_____ au taadhima ni jambo azizi _____2_____kwa mwanafunzi yeyote ambaye hatataka _____3__ ___ katika masomo yake. Mwanafunzi yule ambaye _____4_____ kupiga hatua na kuendelea mbele na masomo yake. Kwa mfano, mwanafunzi anayetaka kuandika insha akhiyari ni sharti azingatie sana _____5_____ ambayo ni mambo _____6_____ yanayoelezewa katika masimulizi au hadithi. Sehemu hii hulenga alama nyingi _____7_____ sehemu nyingine _____8_____ katika mtihani wowote wa uandishi wa insha.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. Nidhamu | B. Taadhimu | C. Azima | D. Azimia |
| **2.** | A. zaidi sana | B. hususan | C. sana zaidi | D. zaidi |
| **3.** | A. kukosa yamini | B. kugonga ndipo | C. kukosa fanaka | D. kula mwata |
| **4.** | A. anaazimu | B. hanatarajia | C. anaazimia | D. hanaazimia |
| **5.** | A. maudhui | B. msamiati | C. mtindo | D. mtiririko |
| **6.** | A. mbora | B. nadra | C. muhali | D. muhimu |
| **7.** | A. kuziliko | B. kuliko | C. kuwaliko | D. kualiko |
| **8.** | A. zinazolengwa | B. zisizolengwa | C. zizizolengwa | D. sizizolengwa |

Ni hivi _____9_____tuliposhuhudia _____10_____mingi ya wanafunzi katika shule za upili za mabweni. Hulka hizi zinachochewa zaidi na matumizi ya _____11_____katika shule zetu. Wanafunzi wengi _____12_____ kwa kujihusisha na wenzao walio na nia mbaya. Uchunguzi uliofanywa na washika _____13_____ katika sekta ya elimu unadhihirisha _____14_____ shahiri kuwa huwa wananyimwa muda wa kujieleza. Wanafunzi wana haki na uhuru wa kusikilizwa ili kuelezea _____15___ yao lakini si kwa kujichomea malazi yao wenyewe.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **9.** | A. majuzi | B. juzi | C. juzijuzi | D. maajuzi |
| **10.** | A. mikosi | B. vigomo | C. migomo | D. mikomo |
| **11.** | A. madawa ya kulevya | | B. madawa za kulevya | |
| | C. mihandarati | | D. dawa za kulevya | |
| **12.** | A. hufuata nyuki ili kula asali | | B. hula janga na wa kwao | |
| | C. huambulia patupu | | D. huwa bendera inayofuata upepo | |
| **13.** | A. dua | B. dau | C. doria | D. dohari |
| **14.** | A. dahiri | B. dhahiri | C. dhati | D. dhana |
| **15.** | A. maoni | B. matakwa | C. malalamishi | D. lalama |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu sahihi.***

**16.** Tambua sentensi iliyoakifishwa barabara.

A. Mama alienda sokoni akanunua; mayai, nyanya, vitunguu na mboga

B. Wanafunzi wote-waliopata alama mia nne-walipata ualishi shereheni.

C. Chakula kama vile mizizi, mbegu, nafaka, na matunda vina virutubishi muhimu mwilini.

D. Mwalimu wangu (wa Kiswahili) anapenda mashairi

**17.** Andika wingi wa sentensi ifuatayo:

***Mkunga aliyevuliwa aliliwa na kobe.***

A. Mikunga waliovuliwa waliliwa na makobe.

B. Wakunga waliovuliwa waliliwa na kobe.

C. Mikunga iliyovuliwa ililiwa na makobe.

D. Mikunga waliovuliwa waliliwa na makobe.

**18.** Chagua sentensi yenye kivumishi cha pekee

A. Mtoto mzuri ni yule mtiifu.

B. Nyumba safi hukalika vyema.

C. Rais aliwatimua wale waliokuwa na rekodi ya ufisadi.

D. Nyanya haruhusiwi kula chakula chochote chenye sukari.

**19.** Ni sentensi gani kati ya zifuatazo iko katika hali tegemezi?

A. Mfumo mpya wa masomo umeanza kutekelezwa.

B. Ungefika mapema ungemfikia mgeni mashuhuri.

C. Hajaja na karo kama alivyoagizwa na hedimasta.

D. Wakenya wa magharibi hupendelea sana kula sima.

**20.** Majira ya mvua ndogondogo kati ya Julai ma Oktoba katika kanda ya Afrika Mashariki huitwaje?

A. Kipupwe

B. Kiangazi

C. Kifuko

D. Mchoo

**21.** Ni ugonjwa gani kati ya magonjwa yafuatayo usiohitaji chanjo kwa watoto wasiozidi miaka mitano?

A. Kifuakikuu

B. Seneneko

C. Ukambi

D. Kifaduro

**22.** Nilikuwa nimelala kifudifudi niliposikia sauti upande wangu wa kushoto. Iwapo kichwa changu kilielekea mashariki, sauti ilitoka upande gani?

A. Kusini

B. Magharibi

C. Mashariki

D. Kaskazini

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu sahihi.***

**16.** Tambua sentensi iliyoakifishwa barabara.

A. Mama alienda sokoni akanunua; mayai, nyanya, vitunguu na mboga

B. Wanafunzi wote-waliopata alama mia nne-walipata ualishi shereheni.

C. Chakula kama vile mizizi, mbegu, nafaka, na matunda vina virutubishi muhimu mwilini.

D. Mwalimu wangu (wa Kiswahili) anapenda mashairi

**17.** Andika wingi wa sentensi ifuatayo:

***Mkunga aliyevuliwa aliliwa na kobe.***

A. Mikunga waliovuliwa waliliwa na makobe.

B. Wakunga waliovuliwa waliliwa na kobe.

C. Mikunga iliyovuliwa ililiwa na makobe.

D. Mikunga waliovuliwa waliliwa na makobe.

**18.** Chagua sentensi yenye kivumishi cha pekee

A. Mtoto mzuri ni yule mtiifu.

B. Nyumba safi hukalika vyema.

C. Rais aliwatimua wale waliokuwa na rekodi ya ufisadi.

D. Nyanya haruhusiwi kula chakula chochote chenye sukari.

**19.** Ni sentensi gani kati ya zifuatazo iko katika hali tegemezi?

A. Mfumo mpya wa masomo umeanza kutekelezwa.

B. Ungefika mapema ungemfikia mgeni mashuhuri.

C. Hajaja na karo kama alivyoagizwa na hedimasta.

D. Wakenya wa magharibi hupendelea sana kula sima.

**20.** Majira ya mvua ndogondogo kati ya Julai ma Oktoba katika kanda ya Afrika Masharika huitwaje?

A. Kipupwe

B. Kiangazi

C. Kifuko

D. Mchoo

**21.** Ni ugonjwa gani kati ya magonjwa yafuatayo usiohitaji chanjo kwa watoto wasiozidi miaka mitano?

A. Kifuakikuu

B. Seneneko

C. Ukambi

D. Kifaduro

**22.** Nilikuwa nimelala kifudifudi niliposikia sauti upande wangu wa kushoto. Iwapo kichwa changu kilielekea mashariki, sauti ilitoka upande gani?

A. Kusini

B. Magharibi

C. Mashariki

D. Kaskazini

**23.** Geuza katika usemi halisi:

*Ami alimwambia halati kuwa asingemfahamisha siku hiyo.*

A. "Sitakufahamisha siku hiyo," ami alimwambia halati.

B. "Sitakufahamisha leo," ami alimwambia halati.

C. "Ami alimwambia halati kuwa," asingemfahamisha siku hiyo.

D. "Sitakufahamisha leo," halati alimwambia ami.

**24.** Chagua mpangilio mzuri wa nyakati

A. Majuzi, juzi, jana, leo, kesho, keshokutwa.

B. Leo, kesho, keshokutwa, mtondo, majuzi, jana, juzi.

C. Jana, juzi, majuzi, mtondo, mtondogoo, kesho, leo.

D. Leo, mtondo, kitojo, mtondogoo, jana, majuzi, kesho, keshokutwa.

**25.** Maamkizi **'chechei'** hujibiwaje?

A. Ewaa

B. Majaliwa

C. Jaala

D. Chewa

**26.** Chagua kielezi cha kutilia mkazo kinachotoa maana ya <u>siku zote.</u>

A. Tangu asili na jadi

B. Usiku kucha

C. Utu na mtu

D. Daima dawamu

**27.** Ni sentensi gani isiyo sahihi?

A. Garini mle kumefunguliwa.

B. Garini kule kumefagiliwa.

C. Gari lile limefagiliwa.

D. Garini pale pamefagiliwa.

**28.** <u>'Kwa"</u> imetumikaje katika sentensi ifuatayo?

<u>Kwa</u> nyanya watu hula ugali <u>kwa</u> maziwa.

A. umilikaji, umilikaji

B. umilikaji, pamoja na

C. kiwakilishi, umilikaji

D. kielezi, mahali

**29.** Ni methali ipi isiyofaa kuwa katika kundi hili?

A. Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.

B. Damu ni nzito kuliko maji.

C. Afadhali ndugu mui kuliko rafiki mzuri.

D. Udugu ni kufaana si kufanana.

**30.** Jua huzama kuelekea magharibi wakati wa

A. Magharibi

B. Adhuhuri

C. Macheo

D. Alasiri

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40***

Utalii ni sekta muhimu katika taifa letu ambayo haifai kupuuzwa hata kidogo. Taifa la Kenya liko kwenye ramani ya utalii duniani na hupokea watalii wa ndani kwa ndani, wa kutoka nchi nyingine za Afrika na isitoshe, duniani. Nchi hii hupokea watalii kutoka mabara kama vile: Ulaya, Asia, Amerika na Australesia. Pesa za kigeni tunazozipokea zinatusaidia sana kupiga hatua kiuchumi kama taifa. Hata hivyo, mikakati kabambe inafaa kuwekwa na washikadau wote ili kuinua sekta hii hata zaidi.

Nchi ya Kenya ina mazingira mema na yenye kuajabia sana. Kwa mfano, kuna mbuga za wanyama zenye wanyama kama vile simba, tembo, chui, kifaru na ndege mbalimbali. Vilevile, pwani yetu yenye mchanga na maji yenye burudani, hoteli zenye mashiko ya kufurahisha, miti ya kiasili na tamaduni za kiafrika zenye rutuba ya kupendeza ulimwenguni. Ni mandhari yenye kupigiwa mfano kwa hakika.

Ni kwa nini tunahimiza taifa kuzingatia sekta hii? Ni kwa sababu utalii ni uti wa mgongo wa uchumi wa taifa hili. Watalii wanapozuru hutupa faida isiyo na kifani. Mwanzo ada wanazolipa ili kuingia mbugani, pili ajira kwa viongozi wa watalii hawa, tatu hoteli wanapojisetiri na kula vyakula na vilevile magari maalum ya kitalii yanayowabeba kutoka sehemu moja hadi nyingine. Tunaweza kusema kuwa kuichochea sekta ya utalii ni kutumia jiwe moja kuua ndege kadhaa. Wananchi wa Kenya pia wanahimizwa kutembelea maeneo ya kitalii ili nao kufahamu vivutio vilivyo nchini. Iweje mzungu atoke Ulaya kutazama simba ilhali mwananchi mzalendo hajamwona simba ambaye yuko kwao? Kumbuka kuwa ada za watalii wa ndani kwa ndani zimepunguzwa karibu na bure.

Kuna mambo kadhaa yanayoweza kufanywa ili kuinua sekta hii muhimu. Mwanzo ni kuimarisha miundo msingi kama barabara, stima, maji na pia usalama wa watalii kuangaziwa zaidi. Ni jambo la kuvunja moyo kusikia kuwa watalii wamesumbuliwa katika maeneo fulani nchini mwetu. Hayo ni mambo ambayo huipaka nchi yetu tope machoni pa wageni. Ada za utalii vilevile zinafaa kuwa chini kwani nchi hii hung'ang'ania wageni na nchi jirani zenye mazingira kama yetu. Jambo adhimu zaidi ni kufanya matangazo duniani kuhusu vivutio vyetu.

Japo tunapata faida nyingi kutokana na utalii huu, inafaa tufahamu kuwa hakuna mchele unaokosa ndume. Ni jambo la kuhuzunisha kusikia kuwa wapo watalii ambao lengo lao kuu kufika nchini ni kufanya ukahaba. La kuvunja moyo zaidi, wao hulenga watoto walio chini ya miaka kumi na minane. Uhayawani huu ambao umekita mizizi zaidi hususan katika jiji la pwani yetu sharti ukomeshwe kwa vyovyote vile. Ni sharti serikali iingilie kati na kupinga hulka hizi kwa jino na ukucha.

Madhila mengine yanayosababishwa na utalii ni wale watalii wanaoeneza dawa za kulevya kwa vijana wetu wadogo. Utawaona vijana wachanga wa maeneo ya kitalii wakiwa mazuzu kwa kubugia na kuwa waraibu wa mihadarati. Watalii kama hawa, japo wanatuletea fedha, wanafaa kukataliwa au kushikwa na kutiwa ndani kwa kueneza saratani ya mihadarati.

Inafaa tufahamu kuwa vijana ndio viongozi wa kesho na kama taifa ni wajibu wetu kuwakinga dhidi ya mahayawani ambao watajaribu kuharibu mustakabali wao murua. Watalii kama hao wanafaa kupigwa marufuku kukanyaga nchini humu.

31. Watalii ni
A. wazungu wanaoitembelea nchi yetu na kutupa pesa za kigeni.
B. watu wa mataifa ya nje wanaotembelea nchi yetu na kutuletea fedha.
C. wazungu wanaotoka Marekani na Asia kuja nchini kujionea wanyama tofautitofauti.
D. watu wowote wanaoitembelea nchi kwa ajili ya starehe na kuona mazingira kwa ada maalum.

32. Neno **'washikadau'** limetumiwa katika ufahamu kumaanisha
A. watalii pekee
B. walimu pekee
C. watu wanaoitembelea nchi
D. wanaohusika katika sekta ya utalii

33. Kwa mujibu wa kifungu ulichokisoma lengo kuu la utalii nchini ni
A. kustarehe wageni wanaotutembelea
B. kupata sifa za wageni wengi nchini
C. kuinua uchumi wa nchi husika
D. kufanya ukahaba na kuuza mihadarati

34. Kwa nini sekta ya utalii inamithilishwa na jiwe moja linalotumiwa kuua ndege kadhaa?
A. Watalii hulipia mambo mengi mbali na vivutio.
B. Watalii huleta pesa nyingi sana kwa kuzuru wanyama.
C. Watalii huwa wengi na wanaotoka nchi zaidi ya moja.
D. Watalii huchukua hata nafasi ya wenyeji kuzuru.

35. Ni kwa nini wananchi wazalendo vilevile wanahimizwa kutalii nchi yao?
A. Ili kuweza kumwona simba
B. Kuvifahamu vivutio vya utalii
C. Ili kuweza kuleta pesa nyingi
D. Ili kuweka mikakati imara ya utalii

36. Ni vivutio gani ambavyo havikuangaziwa kwenye ufahamu uliousoma?
A. Milima ya Kenya inayovutia.
B. Wanyama kama vile simba na chui.
C. Hoteli zetu zinazowasitiri wageni.
D. Ufuo wenye mchanga na maji ya burudani.

37. Mwandishi amezungumzia mbinu mbalimbali ya kuweza kuimarisha sekta ya utalii. Ni ipi muhimu sana kulingana naye?
A. Kuimarisha usalama katika mazingira ya utalii.
B. Kutazama ada zinazotozwa na kuzifanya ziwe za kirafiki.
C. Kuimarisha miundo msingi katika sekta nzima.
D. Kufanya matangazo kuhusu vivutio vyetu kwa wageni.

38. Si kweli kusema kuwa
A. utalii haujapanua sekta nyingi nchini.
B. utalii umeendeleza mihadarati na ukahaba.
C. watalii pia ni washikadau muhimu.
D. utalii ni uti wa mgongo wa nchi yetu.

39. Mambo ambayo huathiri sana vijana kutokana na utalii ni
A. pesa za kigeni na ukahaba
B. ulevi na mihadarati
C. mambo ya anasa na mihadarati
D. unywaji pombe haramu na ukahaba

40. Ni kwa nini taifa linafaa kuwalinda vijana dhidi ya uozo wa utalii?
A. Vijana hawajatimu umri wa ukahaba na mihadarati
B. Watoto wadogo hawafai kuharibika mapema
C. Vijana ni viongozi wa kesho na mustakabali wao unafaa kuchungwa
D. Vijana hawajafikia umri wa kujiamulia mambo yao wenyewe.

***Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali 41-50.***

Maua alikuwa ameshukiwa na nyota ya jaha kwani alipata kibarua cha kuwapikia wafanyakazi chai katika kampuni ya WATALA. Ilikuwa kampuni iliyotengeneza nguo za pamba zilizouzwa ughaibuni. Ni katika mazingira hayo ya kazini ambapo alivutiwa na mtanashati aliyefanya kazi ya uhasibu katika kampuni hiyo. Usuhuba wa wawili hawa ulipelekea kuzaa matunda ya akidi. Bwana Mtali alipendwa sana pale kazini kutokana na heshima, bidii na uchangamfu aliokuwa nao kazini. Alipendwa na kupendelewa zaidi na bosi wake kwani alikuwa mwadilifu na mwaminifu machoni pa mwajiri wake.

Wazazi hawa wachanga walibarikiwa na mtoto aliyekuwa gashi. Kwa kuwa wazazi wake walivuna donge nono, mwana huyu alilelewa kwa tunu na tamasha. Aliishi maisha ya starehe kwani alikuwa na vitu vingi kuliko alivyohitaji. Maadamu baba yake mwana aliyapenda na kuyathamani masomo alimpeleka mwanawe katika shule ya kutajika ambayo hakuna fukara ambaye angeweza kuweka guu lake kule. Mtoto huyu wa kipekee; Mwali, hakuwa na budi ila kuwa na kiburi na maringo. Isitoshe, Maua alijinata na kujipiga kifua kwa kuwa mke wa mwenye pesa na kuwaona wengine kama wasiofaa. Kamwe hakuvalia nguo zilizotengenezwa nchini. Mavazi yake yote yaliagizwa kutoka Ujerumani.

Pale kazini palikuwa na wafanyakazi wa umri mkubwa ambao walikuwa wamefanya kazi kwa muda mrefu bila ya kupata madaraka. Waja hawa hawakumpenda Mtali hata kiduchu; walimwonea gere. Kila mara walisikika wakisema, "Sisi hatutakuwa hapa kwa muda wote huu hapa na kisha kikembe kiletwe kuogelea kwenye pesa zetu." Hayo yalikuwa matamshi ya Bwana Mfaki aliyekuwa msaidizi wa Bwana Mtali. Hawakuelewa fika kuwa Bwana Mtali alikuwa kwenye afisi hiyo kwa mintarafu ya kisomo chake cha chuo kikuuu. Watu wengi mahali pale walitarajia kupata madaraka kwa kuwa na tajiriba ya utendakazi kwa muda mrefu.

Siku moja mgogoro ulizuka pale kazini. Kiasi kikubwa cha pesa kilikuwa kimepotea kwa njia iliyokuwa ya kutatanisha. Kwa kuwa Bwana Mtali ndiye aliyekuwa mhasibu mkuu, alihusishwa na kashfa hiyo. Ilibidi amwage unga na baadaye kufunguliwa daawa. Alisukumana na kesi hiyo kwa zaidi ya nusu mwaka na kwa bahati mbaya wakili wake walishindwa kumtetea ipasavyo na kwa hivyo akashindwa kesi. Alipigwa faini ya shilingi milioni tatu zilizopotea awali. Kwa kuwa akaunti yake haikuwa na pesa za kutosha, ilimbidi auze bidhaa za thamani alizokuwa nazo ili asije akala kalenda kwa miongo miwili na nusu.

Umaskini ukaivaa familia ile ambayo awali ilikuwa yenye ukwasi mkubwa. Maisha ya ukata yaliwavamia vaa bin vuu. Aidha, upendo kwenye familia ukaanza kupoa. Bi Maua akageuka na kuwa mwenye matusi, rabsha na dharau katika nyumba ile. "Wewe ni mume wa aina gani hasa? Yaani hutaweza kulinda na kulea familia yako? Mimi sitakubali kumlisha mume mwizi na mvivu," mke wa mtu alimvamia mumewe. Maji yalipozidi unga, Maua aliitisha talaka na kumfukuza mumewe ambaye alikaribishwa na rafiki yake aliyeishi katika jiji kuu la Rahatule. Aliamua kufanya vibarua na kisha akapata kijumba kidogo cha kukodisha. Pale Rahatule Bwana Mtali alimpata mwanadada mwingine aliyempenda kwa dhati na kujenga familia mpya. Aliamini kuwa kuvunjika kwa mwiko si mwisho wa kupika.

Kwa kuwa Mungu hamwachi mja wake, siku moja Mtali alipata uteuzi wa rais kuwa waziri wa fedha. Matangazo haya aliyapokea kwenye redio na kisha kutazama kwenye runinga. Bwana Mtali alipatiwa jumba kubwa la serikali karibu na ikulu ya rais. Mbali na hayo, alipatiwa ulinzi wa serikali na gari kubwa la aina ya V8 kumpeleka ofisini kila siku. Maua aliposikia habari hizo, alirudi kwa Mtali kwa matao ya chini akimwomba msamaha huku akilia kwi kwi kwi na kujuta. Bwana Mtali alimjibu kwa upole, "Nakubali kukusamehea lakini nafasi yako imechukuliwa na Alice, mke wangu wa dhati."

**41.** Katika aya ya kwanza

A. Maua alipatiwa kazi na Bwana Mtali

B. Mtali na Maua walikuwa marafiki tu basi

C. Marafiki wale wawili walifunga ndoa

D. Maua alikuwa akifanya kazi ya uhasibu

**42.** Ni nini maana ya **kushukiwa na nyota ya jaha**?

A. Kupata mpenzi uliyempenda

B. Kupata kazi kwenye kampuni

C. Kupendwa na mtu mwenye haiba

D. Kupata bahati kubwa

**43.** Mtoto aliyezaliwa baina ya Maua na Bwana Mtali alikuwa wa jinsia gani?

A. Kike

B. Kiume

C. Ghulamu

D. Hatujaambiwa

**44.** Katika aya ya pili, ni kweli kusema kuwa

A. familia ile ilikuwa ya watu walalahoi

B. Maua alionekana akiwa mtu mwadilifu ajabu

C. familia ile ilikuwa ya watu walalahai

D. Maua alipendana na Mtali kwa kuwa alikuwa tausi

**45.** Mtali alikuwa mtu wa aina gani kazini?

A. Mwadilifu, mchangamfu, na mbadhirifu wa mali ya kampuni

B. Mwenye bidii, mwaminifu, kipenzi cha wengi

C. Mbadhirifu, mwaminifu na mwadilifu

D. Mwaminifu, mwenye kuaminika na mwenye kiburi

**46.** Katika kampuni ya Watala

A. watu walipata madaraka kutokana na kisomo chao

B. watu walipata madaraka kutokana na walivyopendwa na bosi wao

C. watu walipata madaraka kutokana na umri wao

D. watu walipata madaraka kutokana na tajriba yao

**47.** Ni nini maana ya msemo **"...amwage unga"**?

A. Kufungwa gerezani

B. Kumwaga unga wa kupikia kazini

C. Kufutwa kazi au kupigwa kalamu

D. Kutalikiana na mke wake

**48.** Iwapo Bwana Mtali hangemudu kulipa faini ile

A. angekula kalenda kwa miaka miwili unusu

B. angefungwa kwa nusu ya mwaka mmoja

C. angekula kalenda na kuuawa gerezani

D. angefungwa gerezani kwa miaka ishirini na mitano

**49.** Habari uliyoisoma inakuelezea wazi kuwa ni nini kilichochochea upendo katika familia ya Mtali na Alice?

A. Uteuzi wake kuwa waziri

B. Mapenzi ya dhati baina yao

C. Kupoteza kazi na kuhurumiwa

D. Pesa zake nyingi alizokuwa nazo

**50.** Kulingana na taarifa, ni bayana kuwa

A. Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe

B. Afadhali rafiki wa karibu kuliko ndugu wa mbali

C. Usiache mbachao kwa msala upitao

D. Damu ni nzito kuliko maji